**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI BALANG'DALALU**
**S. L. P 67**
**KATESH.**
**TAREHE :………………**

**NAMBA ZA SIMU**

- **MKUU WA SHULE 0784-844092**
- **M/MKUU WA SHULE 0755 900058**

**MZAZI/ MLEZI WA WANAFUNZI**
**…………………………………………**
**S. L. P. …………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO**
**SHULE YA SEKONDARI BALANG'DALALU**
**MWAKA 2022**

**1. Utangulizi**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa mwanao………………………………………. amechaguliwa kujiungana kidato cha tano katika shule ya sekondari Balangdalalu mwaka 2022 tahasusi ya **HGL**

Shule hii ipo Halmashauri ya wilaya ya Hanang', Mkoa wa Manayara. Kilometa 22 kusini mwa barabara kuu ya Arusha – Singida

Hivyo unapokuja utashukia stendi ya mabasi ya Katesh nakupanda magari yanayokuja Balangdalalu Sekondari kwa nauli ya shilingi 2000/= tu kwa magari ya abiria.

Muhula wa masomo unaanza mwezi June, 2022,hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 13 June,2022 mwisho wa kuripoti ni siku 14 (kumi na nne) baada ya kufungua shule.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia :**

**Sare ya shule**

a. Sare ya shule ni sketi mbili kwa wasichana na suruali mbili kwa wavulana , mashati mawili, sweta mbili,tai mbili, Tshirt mbili.
b. Sare ya michezo ni bukta ya blue,Tshirt nyeupe isiyo na maandishi, pamoja na raba.
c. Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga gidamu vyenye visigino vifupi
d. .Soksi ndefu pea mbili nyeupe kwa wasichana na soksi nyeusi pea mbili kwa wavulana.

e. Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.
f. Sare ya kazi za nje ni sketi ya khaki kwa wasichana na suruali ya khaki kwa wavulana vyote vinavaliwa na Tshirt ya bluu isiyo na maandishi yenye kola.

**ZINGATIA:**

- **Kipengele hiki cha sare ya shule ni muhimu katika kulinda nidhamu ya shule yetu**
- **Mavazi yote yaliyo orodheshwa hapo juu ndiyo yatakayoruhusiwa kuingia shuleni na si vinginevyo.**
- **VITAMBAA vyote vya kushonea sare ya darasani, masweta, mashati, track suit na Tshirt vinapatikana shuleni.**

**GHARAMA YA SARE YA SHULE**

I. Suruali moja ni Tsh. 22000/=
II. Sketi moja ni Tsh.24000/=
III. Shati moja Tsh.15000/= (mikono mirefu)
IV. Tai 1 Tsh.3500/= ( readymade Tie)
V. Sweta 1 Tsh. 16500/= ( short sleeve lenye nembo ya shule)
VI. Tshirt 1 Tsh.13500/= ( classroom uniform)
VII. Track suit 1 Tsh.25,000/=

*** SARE YA SHULE NI JOZI MOJA MOJA (mbili mbili) ISIPOKUWA TRACK SUIT TU

***** Vyote vilivyotajwa kwenye kipengele (i) hadi (vii) vinapatikana shuleni, vingine vyote ambavyo havikutajwa hapo kwenye sare ya shule nunua uje navyo.**

**3. VIFAA VYA MALAZI**

Kila mwanafunzi aje na:-

- godoro 1 size futi 2.5 upana
- Mashuka 2 ya rangi bluu kwa wavulana na wasichana rangi ya pinki
- Blanketi moja
- Mto 1 wenye foronya inayofanana na shuka
- Chandarua kimoja ili kujikinga na mbu.

**4. VIFAA VYA TAALUMA**

- Kila mwanafunzi aje na madaftari counter books 10 (kumi)
- madaftari madogo ya mazoezi 8 (nane)
- kamusi ya lugha ya kiingereza (Advanced Learners Dictionary)
- vitabu vya msomo ya Tahsusi yako i.e History,Geography,English and General studies.
- kalamu 10, penseli 10, rula ndefu 2
- begi moja la kubebea vifaa vya darasani
- Kila mwanafunzi alete rim paper 1, moja ya photo copy(size A4),

**5. VIFAA VINGINE**

- vyombo vya chakula sahani, bakuli, kikombe,kijiko vyote view vya bati

- uje na ndoo 2 moja kubwa na moja ndogo
- uje na jembe moja lenye mpini
- uje na ufagio chelewa mmoja
- ufagio dekio (mop) moja
- uje na BIMA ya afya kwa ajili yako.

6. ADA YA SHULE

- Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= (elfu sabini tu), unaweza kulipa yote au kwa muhula yaani Tsh.35,000/= (elfu thelathini na tano tu)
- **Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule namba 41001200091, jina la akaunti ni Shule ya Sekondari Balang'dalalu (kumbuka jina la mwanafunzi kwenye slip ya benki)**

**7.** MICHANGO INAYOTAKIWA KULIPWA NA WAZAZI**:**

I. Tsh.15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani za shule hulipwa mara moja
II. Tsh.6000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha hulipwa mara moja
III. Tsh.20,000/= kwa ajili ya taaluma kwa mwaka
IV. Tsh. 40,000/= kwa ajili ya walinzi na vibarua wengine, unaweza lipa kwa muhula Tsh.20,000
V. Tsh. 2000/= kwa ajili ya nembo ya shule
VI. Tsh 20,000/= kwa ajili ya mitihani ya kujipima ya Utamirifu (mock),hulipwa mara moja tu
VII. Tsh. 5000/= kwa ajili ya tahadhari (haitorejeshwa)
VIII. Tsh. 5000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza

- **MICHANGO YOTE ILIPWE BENKI YA NMB**
- **AKAUNTI NAMBA 41001200091**
- **JINA LA AKAUNTI NI SHULE YA SEKONDARI BALAN'DALALU**
- **Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye slip ya benki wakati unalipa**

8. **MAAGIZO**

- Kila mwanafunzi lazima asome sheria , kanuni na taratibu za shule kwa uangalifu azifuate na kuzitii . Kutofanya hivyo ni makosa.
- Uvunjaji wa sheria yoyote ya shule hata ikiwa ndogo kiasi gani hautavumiliwa
- Mwanafunzi lazima ahudhurie vipindi vyote na afanye mazoezi na mitihani ya masomo yote yanayofundishwa darasani kwake. Ni kosa linaloweza kumfukuzisha mwanafunzi shuleni kwa kuacha kuhudhuria vipindi na kuacha kufanya mazoezi / mitihani bila sababu za msingi.

**Sheria za Bweni**

a. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kuchemsha/ kupika bwenini aidha kwa kutumia moto wa kuni, mkaa , mafuta ya taa au moto wa umeme.
b. Bwenini ni mahali pa kulala si pa kupiga kelele. Mazungumzo ya bwenini yawe mazungumzo ya maana na yawe ya sauti ndogo . Upigaji kelele au mayowe ni viashiria vya uhuni, fujo, n.k. hiyo haikubaliki

c. . Usafi wa bweni ndani na nje ( mazingira yanayozunguka bweni ni wajibu wa kila mkaaji wa bweni husika)
d. Ni makosa kukaribisha mgeni wa aina yoyote bwenini au katika eneo la bweni
e. Vyoo vyote lazima vitumike vizuri na kuwekwa katika hali ya usafi
f. Ni wajibu wa viongozi wa bweni pamoja na wana – bweni wote kulinda sheria kwa kuzitekeleza kwa vitendo.
g. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki bwenini vyombo vifuatavyo:- **Redio , pasi, Heater, Kamera ,Simu ya mkononi , Hot pot, Walk man au kifaa chochote cha muziki , Sufuria , Pombe , Madawa ya kulevya , manukato (perfume).**

**NB: Mwanafunzi atakayekutwa na vitu tajwa hapo juu atachukuliwa hatua kali. Unaweza kuja na chupa ndogo ya chai ( Thermos)**

**VIAMBATANISHO MUHIMU VYA KUJA NAVYO SHULENI**

- Fomu ya mapokezi na utambulisho (Joining Instruction Form)
- Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical examination form) **IJAZWE NA HOSPITALI YA SERIKALI**
- Hati ya utii na sheria.Cheti cha matokeo ya kidato cha nne (results slip)
- Picha passport size 3

**Tafadhali soma kwa makini Sheria za shule zilizoambatanishwa na Fomu hii**

**KARIBU SANA BALANG'DALALU SEKONDARI**

***YUDA A. FISSOO***

**MKUU WA SHULE**

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENTS**

BALANG'DALALU SECONDARY SCHOOL.
P. O. BOX 67,
KATESH.
HANANG-MANYARA
DATE:…………………

REF: NO. BSS/MED/VOL.I/2021.

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM.

TO THE MEDICAL OFFICER, …………………………………………………..…..

……………………………………… ……………………………………….

Please examine ………………………………………………(Name of students)
Who has been selected to join this school for his fitness as a student in the following:-
(To be completed by a medical officer)

1. Eye sight …………………………..
2. Hearing……………………………
3. Limbs………………………………
4. SPECIMEN i) Stool………………… ii) Urine………………… iii) Blood………………… iv) Neurosis………………..
5. Asthma……………………………
6. Tuberculosis ………………………
7. Pregnancy …………………………
8. Other serious disease:- i) Venereal disease…………………….. ii) Leprosy ……………………….. iii) Epilepsy ……………………. iv) Ulcers………………………

MEDICAL CERTIFICATE:
(To be completed by a Medical Officer) I have examined the above and consider him/ her to be physically fit / unfit as a student .
Date: …………………………… Signature: …………………………………
Station : …………………………… Designation:………………………………

NB: I request this form to be returned to the school in a sealed – envelop.

……………….………..
**THE HEADMASTER**

**FOMU YA MAPOKEZI SHULENI**

**MAELEZO KUHUSU MWANAFUNZI ( IRUDISHWE SHULENI)**

**SEHEMU: "A" – Ijazwe na mwanafunzi;**

**Jina la Mwanafunzi ( majina matatu) …………………………………………………………**

**Anwani; ……………………………………………………………..**

**Taifa / Uraia : …………………………………………………………..**

**Dini : ………………………………………………………………………..**

**Tarehe ya kuzaliwa :……………………………. Jinsia :………………..**

**Shule anakotoka (Shule ya Sekondari ) :…………… ………………..Kata ya ………….**

**Mwaka wa kumaliza kidato cha nne : …………………………………………………..**

**Wilaya anakotoka :………………………………………………………………………….**

**Mkoa :………………………………………………………………………………..**

**SEHEMU "B" ( Ijazwe na mzazi/ mlezi)**

**Jina la mzazi / mlezi (majina matatu)**

**……………………………………………………………………………………….**

**Anwani ya mzazi/ mlezi :……………………………………………………….**

**Namba ya simu ya simu ya mzazi / mlezi………………………………………**

**Mahali anapoishi : ………………………………………………………………………**

**Kazi ya mzazi / mlezi…………………………………………………………**

**Mahali anapofanya kazi : ……………………………………………………………….**

**Ndugu wawili wa karibu ( wanaoweza kushika nafasi ya mzazi / mlezi )**

**SEHEMU "C"**

**d) Tafadhali fika na vifaa vyote ulivyoagizwa**

**e) Wahi shuleni kabla ya saa 11:00 jioni**

**f) Mzazi hakikisha unakamilisha malipo yote kabla ya kumleta mwanao shuleni .**

**………………………………..**

**SAHIHI YA MZAZI/ MLEZI**

**……………………….**

**SAHIHI MKUU WA SHULE**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI BALANG'DALALU**

**KIAMBATANISHO "A**

**FOMU YA KUKUBALI**

**MWANAFUNZI AJAZE SEHEMU HII:**

Mimi ……………………………………………..msichana/mvulana ninakubali kuingia kidato cha kwanza shule ya Sekondari Balan g'dalalu.

Tarehe…………………na nitafika shuleni bila kuchelewa.

Nitatii sheria za shule na nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kwenye kazi za nje. Mungu nisaidie.

Anwani yangu ya kudumu Ni

______________________________

3.Sahihi ya mwanafunzi_____________________

**<u>MZAZI/MLEZI AJAZE SEHEMU HII</u>**

Mimi …………………………………………………nakubali

Mtoto wangu………………………………………(jina) asome katika shule ya sekondari Balang'dalalu.

Naahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyooneshwa katika barua ya masharti ya kujiunga na shule hii.

Naahidi kuwa nitamsihi kutii sheria zote za shule na kuwa na bidii kwenye masomo na kwenye kazi za nje pia.

Anwani yangu ya kudumu ni

_______________________________

_______________________________

_______________________________

Sahihi ……………………………………………………………tarehe …………….

**Wageni ninaowaidhinisha kuja kumwona mwanangu awapo shuleni muda maalumu ulio pangwa na shule ni kila Jumamosi na Jumapili za mwisho wa miezi tu.(Wasizidi wawili)**

| JINA | UHUSIANO |
|---|---|
| __________________________________ | _______________________________________ |
| __________________________________ | _______________________________________ |

## OFISI YA RAIS TAMISEMI

### SHULE YA SEKONDARI BALANG'DALALU

**S.L.P 67**

**KATESH**

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.**

Sheria za Shule zina lenga katika kumlea mwanafunzi awe na nidhamu, azingatie maadili ya Taifa letu na hatimaye aishi kama raia mwema anayekubalika na jamii yetu. Ni imani yetu kuwa shule yenye wanafunzi wenye nidhamu hufanya vizuri katika taaluma.

Shule yetu inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978 na marekebisho yake yote. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu hapa Tanzania. Kwa ajili ya ufanisi, unatakiwa kuzingatia sheria na kanuni hizi kwa kipindi chote utakachokuwa hapa shuleni.

**HIVYO NI LAZIMA KWA KILA MWANAFUNZI WA SHULE HII.**

1. Kuhudhuria masomo kila siku, tatizo la ugonjwa, msiba nk litaombewa ruhusa.
2. Kuzingatia wastani wa ufaulu unaowekwa na shule na mabadiliko yake yote.
3. Kusalimu watu wote na hasa waliomzidi umri
4. Kusimama mwalimu anapoingia darasani au wakati wa kuuliza na kujibu swali.
5. Kuvaa nguo za heshima shuleni na hata nyumbani
6. Kutii sheria zote za shule
7. Ni muhimu kutunza usafi wako binafsi na mazingira ya shule
8. Kukaa kimya na nidhamu darasani
9. Mwanafunzi huruhusiwi kutembea usiku bila sababu yoyote.
10. Daima uwe msafi kimwili na mavazi.Uwe na nywele fupi,kufuga ndevu au masharubu hairuhusiwi shuleni.
11. Ni marufuku mwanafunzi kujiunga na vilabu vya michezo nje ya shule
12. Ni marufuku kwa mwanafunzi kushiriki katika vigenge vya usengenyaji au kusema uongo.
13. Usifanye biashara aina yoyote shuleni.
14. Usichelewe siku za kufungua shule au usiongeze siku za ruhusa.
15. Usikatae uteuzi wa kushiriki shughuli za Shule.
16. Usigune wakati mwalimu au kiongozi yoyote anapotoa tangazo kama kuna swali nyosha mkono, utaratibu ufuatwe.
17. Usibandike au kuandika tangazo lolote lile bila ruhusa ya mwalimu anayehusika.
18. Kutumia lugha chafu kama matusi n.k

19. Kufuga kucha, nywele ndefu, kuvaa mikufu, kupaka marashi au rangi kwenye kucha au kuvaa hereni, kuwa na kamera, redio, simu ya mkononi awapo shuleni.
20. Kufanya mapenzi na wanafunzi wenzake au watu wengine nje na ndani ya shule
21. Kuambatana na makundi ya wahuni wa mitaani
22. Kuondoka shuleni kabla ya muda wa masomo kuisha (utoro).
23. Mwanafunzi anatakiwa kuonesha bidii na akiwa shuleni atashiriki shughuli zote watakazoshiriki wenzake kama vile kufanya usafi wa mazingira na shughuli zingine zitakazoelekezwa na uongozi wa shule.
24. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa mtii, kujiheshimu yeye binafsi na kuwaheshimu watu wengine: walimu, wafanyakazi wa shule, viranja pamoja na wanafunzi wenzake.
25. Ni muhimu na wajibu kwa kila mwanafunzi kuwahi mahali popote atakapohitajika: darasani, mihadharani, michezoni na kazini.
26. Ni marufuku kwenda nje ya eneo la shule bila ruhusa ya uongozi unaohusika.
27. Mgeni yeyote lazima atambulishwe kwa Mwalimu wa Zamu kabla ya kukaribishwa kumwona mwanafunzi.
28. Siku ya Wazazi kuwaona watoto wao itakuwa kila jumamosi na Jumapili ya kila wiki kwa wazazi wote. Ni marufuku kwa mzazi yeyote kumletea mtoto wake chakula cha aina yoyote (na vitu vingine haramu katika mazingira ya shule, kwani kitendo hicho kitaambatana na kumchukua mtoto kurudi naye nyumbani.
29. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuonekana ndani au kwenye mazingira ya nyumba za kulala wageni/hoteli.
30. Kila mwanafunzi ni lazima atunze ukimya muda wote awapo darasani, maktaba, chumba cha kompyuta na mahali popote atakapotakiwa kufanya hivyo.
31. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kutunza siha na usafi wake binafsi na wa mazingira yote ya shule.
32. Kila mwanafunzi atawajibika kulinda na kutunza mali ya shule na yake binafsi. Mwanafunzi atakayeharibu mali ya shule atapaswa kulipa mara moja baada ya kuthibitika.
33. Lugha ya mawasiliano mwanafunzi awapo shuleni ni Kiingereza. Kiswahili kitatumika katika vipindi vya somo hilo darasani, wakati wa kujadiliana somo hili katika vikundi vya kujisomea na matukio maalum kama itaamriwa hivyo na uongozi husika.
34. Kubaki nyumbani kwa sababu ya ugonjwa hakutakuwa na msamaha wowote endapo mwanafunzi hakupewa ruhusa kimaandishi. Mwanafunzi asiyefika shuleni pasipo ruhusa atahesabiwa kuwa mtoro tendo ambalo baadaye linaweza kusababisha kuondolewa shuleni.
35. Ugomvi au kupigana, kuleta fujo darasani au eneo lolote la shule, lugha chafu na matusi, kashfa kwa wenzako au raia ni mwiko kabisa. Shuleni ni mahali pa kuheshimiana, vitendo vya unyanyasaji wa madarasa ya chini na wageni havitavumiliwa.
36. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kutumia vitu ambavyo vitamwingizia gharama isiyokuwa na umuhimu kama vile matumizi ya vipodozi, kusuka nywele, kupaka wanja, kupaka rangi kucha, na mitindo mbalimbali ya wanaume ya kunyoa nywele. Kwa wasichana ni marufuku kusuka nywele.
37. Wizi ni kosa kubwa sana. Adhabu yake ni kufukuzwa shule.

38. Vitendo vyovyote vya kushiriki au kushawishi mgomo wa aina yoyote shuleni adhabu yake ni kufukuzwa shule.
39. Siku zote awapo shuleni mwanafunzi atakula chakula kitakachopatikana ndani ya eneo la shule tu na kitaliwa sehemu husika na si mahali pengine.
40. Kila mwanafunzi ni lazima avae sare ya shule muda wote awapo ndani ya eneo la shule isipokuwa kwa kesi maalum itakayothibitishwa na uongozi.
41. Nyumba za watumishi ni nje ya eneo la shule. Ruhusa maalum itafutwe kutoka kwa Mwalimu wa Zamu au Mshauri wa Wanafunzi (Patron/Matron) kama kuna umuhimu wa mwanafunzi kufika huko muda wa shule au muda mwingine wowote.
42. Redio, simu za mkononi, camera na vifaa vyovyote vya umeme haviruhusiwi kabisa shuleni. Pia hairuhusiwi kuunganisha au kung'oa sockets, switch au bulbholders au nyaya za umeme popote pale katika majengo ya shule au sehemu za kulala.
43. Adhabu: Mwanafunzi akivunja mojawapo ya kanuni za mwenendo bora anaweza kupewa adhabu na Kiongozi wake (mwanafunzi) au Mwalimu kutegemea uzito wa kosa.
44. Dini: Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kujishughulisha na kuhubiri itikadi za dini awapo shuleni, wala kuudai uongozi utimize taratibu na sera za dini au dhehebu lake.

- Fedha za mkononi: Hakuna mwanafunzi atakayeruhusiwa kukaa na fedha. Fedha zote zitakabidhiwa kwa Mwalimu wa malezi na zitatumika kwa ridhaa ya mwanafunzi mwenyewe kimaandishi au mzazi ikiwa ni jambo muhimu.
- Malipo: Malipo yote yatafanyika benki. Shule haitampokea wala kushughulikia kesi ya mwanafunzi yeyote itakayosababishwa na huduma ya benki kama vile upokeaji wa risiti feki.

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE**

I. Wizi
II. Mapenzi, ubakaji na ushoga
III. Ulevi wa aina yoyote, pombe au madawa ya kulevya
IV. Uvutaji bangi
V. Makosa ya Jinai
VI. Kupigana au kupiga
VII. Kukataa adhabu
VIII. Kuoa au kuolewa
IX. kusababisha ujauzito kwa mwanafunzi mwenzako/kumpa ujauzito mtu yeyote asiye mwanafunzi
X. Ujauzito na kutoa mimba
XI. Kuharibu kwa makusudio mali za umma
XII. Kudharau bendera au wimbo wa taifa
XIII. Kufanya, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au kuhatarisha amani ya shule wakati wowote ule.
XIV. Kukataa kutii amri ya mkuu wa shule au mwalimu yoyote.
XV. Kutoroka mitihani na mazoezi ya darasani

**MUHIMU**:

Kwa makosa yale yanayovumilika mwanafunzi atapata onyo kimaandishi mara **mbili tu** na mara ya tatu onyo litaambatanishwa na barua ya kufukuzwa shule.

Wako katika Ujenzi wa Taifa

…………………………………..

Yuda A. Fissoo

Mkuu wa Shule

**ZINGATIO:**

MAISHA YA SHULE NI MAZURI KWA WALE TU WATAKAOFUATA SHERIA ZA SHULE. SHULE ITAFUNGULIWA TAREHE …………………………………………FIKA BILA KUKOSA